

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUWASILISHA MAOMBI YA LESENI YA BIASHARA YA NYARA (TROPHY  
DEALER'S LICENCE – TDL) KWA MWAKA 2023**

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) inawajulisha wananchi wenye nia ya kufanya Biashara ya Nyara kuwasilisha maombi yao kwa Kamishna wa Uhifadhi, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Fomu za Maombi ya Leseni zinapatikana katika Ofisi za Wanyamapori za Wilaya, Ofisi za TAWA Makao Makuu Morogoro (Jengo la TAFORI), Ofisi za Utalii na Huduma za Biashara, Dar es Salaam (Gorofa ya 4, Jengo la Mpingo) na ofisi ya Matumizi Endelevu ya Wanyamapori - Arusha zilizopo karibu na ofisi za jeshi la Zimamoto.

Fomu za maombi zinatakiwa kujazwa kwa usahihi, kuwasilishwa na kupitishwa na Maafisa Wanyamapori wa Wilaya. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 Novemba, 2022. Aidha, namba ya malipo (control number) zitatolewa katika Ofisi ya Utalii na Huduma za Biashara Dar Es Salaam na Ofisi ya Matumizi Endelevu ya Wanyamapori Arusha.

***Hakuna Leseni za Daraja lolote kwa mwaka 2023 zitakazotolewa kwa madhumuni ya Ukamataji kwa ajili ya usafirishaji wa Wanyamapori hai nje ya nchi.***

Maombi ya Leseni kwa Mwaka 2023 ni kwa Madaraja yafuatayo:-

<b>Daraja</b>	<b>Maelezo</b>
1	Biashara ya meno ya kiboko au ngiri mazima au kipande ambayo hayajatengenezwa.
2	Biashara ya ngozi za wanyamapori isipokuwa ngozi za pimbi na mbega
3	Biashara ya ngozi za pimbi
4	Biashara ya meno ya kiboko na ngiri ambayo yamenakishiwa
5	Biashara ya kukata na kutengeneza ngozi za chui, simba, mondo au ngozi nyingine za wanyamapori jamii ya paka
6	Biashara ya kukata na kutengeneza ngozi za wanyamapori isipokuwa pimbi na mbega pamoja na kutengeneza vitu kutokana na nyara hizo

7	Biashara za nyara zilizotengenezwa
8	Biashara ya kuhifadhi nyara mbalimbali ili zisiharibike mapema
10	Biashara ya mikia ya wanyamapori isipokuwa ya tembo, faru, na mbega na vitu vinavyotokana na nyara hizo.
11	Wakala wa kusafirisha nyara kwa ujumla isipokuwa wanyamapori hai
17	Bustani ya Wanyamapori
18	Mashamba ya kufuga wanyamapori (isipokuwa kwa nia ya kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi).
19	Vituo vya karantini (isipokuwa kwa nia ya kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi).
20	Ranchi za wanyamapori (isipokuwa kwa nia ya kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi)
21	Aina yoyote ya biashara ya Nyara ambayo haikutajwa kwenye daraja la 1-20 isipokuwa kwa nia ya kusafirisha viumbe hai nje ya nchi. Daraja hili pia linahusisha leseni za uzaji wa nyamapori.

Mwombaji anatakiwa kuwasilisha fomu ya maombi ya leseni pamoja na uthibisho wa yafuatayo:-

1. Endapo mwombaji ni mtu binafsi anatakiwa awasilishe hati ya usajili wa jina la biashara (Certificate of Registration of Business name) au iwapo mwombaji ni Kampuni awasilishe hati ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association) na Hati ya utambulisho wa mlipakodi (Taxpayer Identification Number).
2. Uthibitisho wa kuwa na wakamataji wenye elimu ya uhifadhi wa wanyamapori kutoka kwenye Chuo kinachotambulika na Serikali.
3. Uthibitisho kwamba biashara ina Leseni kutoka kwenye Mamlaka husika.
4. Mpango wa biashara [Business plan] unaohusu biashara inayotarajiwa kufanywa na uthibitisho wa kuwa na mtaji wa kufanya biashara hiyo.
5. Uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi ya leseni ya (TZS 5,000) ambayo haitarudishwa [Non-Refundable].
6. Mwombaji asiwe na rekodi ya kupatikana na hatia ya kuvunja Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009.
7. Kwa waombaji wa shughuli za ufugaji wa wanyamapori, ada ya maombi ya Leseni ya ufugaji itategemea aina ya mradi wa ufugaji kama ifuatavyo:-
  - i. Bustani ya wanyamapori; TZS 30,000/ kwa mzawa, mzawa pamoja na Mgeni TZS 50,000/
  - ii. Mashamba ya ufugaji wanyamapori; ada ni TZS 40,000/ kwa mzawa na kwa mzawa na mgeni ni TZS 100,000/
  - iii. Ranchi za wanyamapori ni TZS 100,000/ kwa mzawa na kwa mzawa na mgeni ni TZS 200,000/

Imetolewa na.

**KAMISHNA WA UHIFADHI  
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA,  
Barabara ya Dar es Salaam,  
Eneo la Kingolwira, Jengo la TAFORI,  
S.L.P 2658,  
MOROGORO  
Simu: 023-2934204  
Barua pepe: cc@tawa.go.tz**